

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA NNE**

**KIKAO CHA TISA**

**10 SEPTEMBER, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA TISA – TAREHE 10 SEPTEMBER, 2021

I. DUA:

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax

III. TAARIFA YA SPIKA:

IV. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

105. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA  
(MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Mapera na Muungano vitaanza kutoa huduma ya upasuaji ambao haufanyiki kutokana na kukosekana kwa baadhi ya vifaa ikiwemo *Sterilizer*.

**106. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA  
KISAU (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule za Sekondari za Lesoit, Dosidosi, Ndedo na Dongo kuwa za Kidato cha Tano na Sita kutokana na uhitaji mkubwa wa Shule za Kidato cha Tano na Sita Kiteto.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA  
UTAWALA BORA):**

**107. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA  
MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutimiza masharti ya ajira kwa Watumishi ikiwa ni pamoja na kuwapandisha madaraja na stahiki nyingine.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **108. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Utalii Nyanda za Juu Kusini katika eneo la Kihesa- Kilolo.

### **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

### **109. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya Akili ya Mirembe ambayo miundombinu yake imeharibika.

**110. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON  
GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imewawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wamepewa jukumu kubwa la kuanzisha na kusimamia shughuli za vikundi vya maendeleo kwenye Halmashauri ili waweze kutimiza majukumu yao ipasavyo.



**WIZARA YA NISHATI:**



**111. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE  
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Mkandarasi wa umeme wa REA ataanza kazi ya kusambaza umeme katika Jimbo la Tunduru Kusini.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **112. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILI ZODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya Wavuvi wa ukanda wa Pwani ili kuchochea uchumi.

### **113. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali imesaidia mikopo kwa vikundi vingapi vya Wavuvi Wilayani Nkasi.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **114. MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganisha Wakulima wa Mikoa ya Kusini hususan Mkoa wa Njombe na Wawekezaji wa nje na ndani.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **115. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaweka Kituo cha Uhamiaji katika eneo la Chipingo ili kuondokana na vivuko bubu vilivyopo Mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **116. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali imewekeza kiasi cha Shilingi Bilioni 20 kwa ajili ya kutengeneza


miundombinu ya ukaguzi wa magari nchini  
(*Destination Inspection*):-

Je, ni sababu zipi zilipelekea Serikali  
kubadilisha mfumo huo.

**117. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI  
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na  
Biashara:-

Je, ni lini Akina Mama zaidi ya 300 waliokuwa  
Wafanyakazi wa Kiwanda cha Kiliflora Wilayani  
Meru watalipwa stahiki zao baada ya Kiwanda  
hicho kufungwa.



**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**118. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO  
(MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na  
Mipango:-

Je, ni nini hatma ya biashara ya maduka ya  
kubadilisha fedha (*Bureau de Change*)  
yaliyofungwa na Serikali.



**119. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA  
KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza Kodi kwenye vifaa vya michezo ili Sekta ya Michezo iweze kustawi.

**V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

**VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

**VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA  
MASHARIKI:**

**DODOMA  
10 SEPTEMBER, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**